**SHERIA YA USAJILI NA USIMAMIZI WA WATAALAMU WA MAABARA ZA TIBA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA AWALI


1. Jina fupi na kuanza kutumika.

2. Ufafanuzi.


### SEHEMU YA PILI
### KUANZISHWA KWA BARAZA NA KAZI ZAKE


3. Kuanzishwa kwa Baraza.

4. Muundo wa Baraza.

5. Kazi za Baraza.

6. Uwezo wa Baraza.

7. Kukasimu uwezo na kazi za Baraza.

8. Kamati za Baraza.

9. Kazi za Kamati.

10. Muundo wa Kamati.


### SEHEMU YA TATU
### UENDESHAJI NA WAFANYAKAZI WA BARAZA


11. Uteuzi wa Mrajis.

12. Sifa za Mrajis.

13. Kazi za Mrajis.

14. Uteuzi, sifa na kazi za Naibu Mrajis.

15. Daftari na machapisho.

16. Maafisa na watumishi wa Baraza.

**SEHEMU YA NNE**
**USAJILI NA LESENI**

17. Maombi ya usajili na kupata leseni.

18. Sifa za usajili.

19. Usajili wa mpito.

20. Usajili wa Muda.

21. Mtu aliyesajiliwa kufanya kazi kwa mujibu wa maadili na miiko ya utendaji.

22. Ukaguzi wa programu za mafunzo ya Maabara ya Tiba.

23. Uteuzi, kazi na uwezo wa Mkaguzi wa Maabara ya Tiba.

24. Mkaguzi wa Maabara ya Tiba atapewa Kitambulisho.

**SEHEMU YA TANO**
**MASHARTI YA NIDHAMU**

25. Mrajis kupokea malalamiko.

26. Uchunguzi wa Baraza.

27. Uwezo wa Baraza wa kuchukua hatua za kinidhamu.

28. Kudharau wito na kukataa kutoa ushahidi.

29. Kuondolewa katika Daftari.

30. Kuwasilisha cheti kuhusiana na kuondolewa jina kutoka katika Daftari.

31. Rufaa dhidi ya kusimamisha utendaji au kuondosha kutoka katika Daftari.

32. Kulirejesha jina baada ya kuondolewa.

33. Masharti ya kurejesha jina katika Daftari.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA FEDHA


34. Vyanzo vya fedha vya Baraza.

35. Hesabu na Ukaguzi.

36. Kutumika kwa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

37. Ripoti ya Mwaka.


## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU


38. Kufanya kazi kinyume na Sheria.

39. Taarifa au nyaraka za udanganyifu.

40. Kuanzisha programu ya teknolojia ya maabara ya tiba.

41. Kujifananisha na kupotosha.

42. Masharti yanayohusiana na utaratibu wa Baraza.

43. Kumuajiri mtu asiyesajiliwa au kupewa leseni.

44. Kusaidia kutenda kosa.

45. Adhabu kwa kumzuia au kumlazimisha Mkaguzi.

46. Machapisho.

47. Adhabu ya jumla.


## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO


48. Ada na tozo.

49. Mtaalamu wa Maabara ya Tiba aliyesajiliwa kutoa huduma bora za maabara ya tiba.

50. Kanuni.


## JADWELI

**SHERIA NAM. 10 YA 2020**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

11 Mei, 2020

# SHERIA YA USAJILI NA USIMAMIZI WA WATAALAMU WA MAABARA ZA TIBA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

*Jina fupi na kuanza kutumika.*

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Wataalamu wa Maabara za Tiba, 2020 na itaanza kutumika baada ya kuwekwa saini na Rais, na kwa tarehe ambayo itatangazwa na Waziri katika Gazeti Rasmi la Serikali.

*Ufafanuzi.*

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"Cheti" maana yake ni hati inayotolewa na Baraza chini ya kifungu cha 19(3) cha Sheria hii;

"Baraza" maana yake ni Baraza la Wataalamu wa Maabara ya Tiba lililoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Serikali" maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Leseni" maana yake ni leseni inayotolewa na Mrajis chini ya kifungu cha 17 (1) cha Sheria hii;

"Mkaguzi wa Maabara ya Tiba" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na Baraza chini ya kifungu cha 23(1) cha Sheria hii;

"Maabara ya Tiba" maana yake ni kituo chochote au chumba ambacho uchunguzi wa kimaabara za tiba unafanywa;

"Mtaalamu wa Maabara za Tiba" maana yake ni mwanasayansi wa Maabara ya Tiba au Mteknolojia wa Maabara ya Tiba aliyesajiliwa na Baraza;

"Mwanasayansi wa Maabara za Tiba" maana yake ni mtu mwenye angalau shahada ya kwanza au stahahada ya juu ya fani ya sayansi ya maabara ya tiba iliyotolewa na chuo cha elimu ya juu kinachotambulika na Baraza;

"Mteknolojia wa Maabara ya Tiba" maana yake ni mtu mwenye stashahada katika fani ya sayansi ya maabara ya tiba iliyotolewa na taasisi ya elimu ya juu inayotambulika na Baraza;

"Uchunguzi wa kimaabara" maana yake ni uchunguzi wa maradhi ambao unafanyika kutoka kwenye sampuli zinazotoka katika mwili wa binaadamu kama vile uchunguzi wa vinasaba, vijidudu vidogo vidogo vinavyoshambulia mwili, maji maji ya damu, kemikali, damu, seli za mwili, kinga ya mwili au aina nyengine yoyote ya uchunguzi au taratibu zinazofanyika katika maabara au hospitali ambazo zinatoa taarifa za magonjwa, kinga au tiba au uchunguzi wa hali ya afya;

"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana za huduma za afya;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Daftari" maana yake ni Daftari la usajili ambalo Wataalamu wa Maabara za Tiba wanasajiliwa;

"Mrajis" maana yake ni mtu ambaye anawasajili Wataalamu wa Maabara za Tiba anayeteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Sheria hii;

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA BARAZA NA KAZI ZAKE

Kuanzishwa kwa Baraza.

**3.**-(1) Kunaazishwa Baraza litakalojulikana kama Baraza la Wataalamu wa Maabara za Tiba.

(2) Baraza litakuwa ni Wakala wa Serikali na litakuwa chini ya usimamizi wa Waziri.

Muundo wa Baraza.

**4.**-(1) Baraza litaundwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mrajis wa Baraza la Wataalamu wa Maabara za Tiba;

(c) Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Uchunguzi katika Wizara ya Afya Zanzibar;

(d) Mtaalamu mwandamizi wa Maabara ya Tiba kutoka katika Chuo kinachotoa Mafunzo ya Maabara kinachotambulika Zanzibar;

(e) Mwakilishi kutoka Jumuiya ya Wataalamu wa Maabara za Tiba;

(f) Mwakilishi kutoka sekta binafsi mwenye uzoefu katika elimu ya sayansi ya Maabara za tiba; na

(g) Wakili wa Serikali kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu.

(2) Isipokuwa Mwenyekiti na wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia uzoefu, utaalamu na usawa wa kijinsia.

(3) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti iwapo mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza ya sayansi ya maabara ya tiba;

(c) ana uzoefu wa kazi angalau wa miaka kumi katika fani hiyo;

(d) ana umahiri wa hali ya juu wa kuendesha mambo ya sayansi za maabara ya tiba kwa ufanisi na ubora; na

(e) ana uadilifu wa hali ya juu.

(4) Mwenyekiti wa Baraza atashika nafasi kwa kipindi cha miaka minne kutoka tarehe ya uteuzi na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

(5) Wajumbe wa Baraza watashika nafasi kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuteuliwa tena kwa kipindi chengine.

(6) Mjumbe aliyeteuliwa kuiwakilisha taasisi atasita kuwa mjumbe wa Baraza mara atakaposita kuwa mtendaji wa taasisi hiyo.

(7) Baraza litamteua Afisa Sheria aliyeajiriwa na Serikali kuwa Katibu wa Baraza.

(8) Taratibu za mikutano ya Baraza na mambo mengine yanayohusiana na Baraza zitakuwa kama zitakavyoelezwa katika Jedweli la Sheria hii.

Kazi za Baraza.

**5.**-(1) Kazi za Baraza zitakuwa ni:

(a) kusajili watu wenye sifa ya kusajiliwa na kutoa hati ya utambulisho au leseni ya kufanyia kazi;

(b) kutoa, kutoa upya, kufuta vyeti au leseni na kurekebisha taarifa zozote zinazohusiana na usajili na kubadilisha cheti au leseni iliyothibitika kuwa imepotea au kuharibika;

(c) kusimamia viwango na utendaji wa taaluma ya Maabara ya tiba;

(d) kufanyisha mitihani kabla ya usajili kwa ajili ya kuhakikisha umahiri wa wataalamu wa maabara ya tiba;

(e) kuhakikisha kwamba Daftari linawekwa, linahifadhiwa na linaingizwa taarifa mpya kwa namna itakavyoelezwa;

(f) kuendeleza mipango mikakati, miongozo ya kisera na taratibu za Baraza;

(g) kuandaa makisio ya bajeti ya mwaka ya Baraza;

(h) kuweka miiko na maadili ya kiutendaji kwa wataalamu wa maabara za tiba;

(i) kuweka viwango na masharti ya kuanzisha programu za mafunzo ya maabara ya tiba;

(j) kuidhinisha na kusimamia mitaala ya ukufunzi na mafunzo ya wataalamu wa maabara za tiba;

(k) kushughulikia malalamiko yaliyowasilishwa dhidi ya Mtaalamu yeyote wa Maabara ya Tiba;

(l) kumshauri Waziri juu ya mambo yanayohusiana na utoaji huduma za maabara za tiba;

(m) kufanya utafiti, mafunzo na mambo mengine yanayohusiana na hayo; na

(n) kutekeleza kazi nyengine zozote au jukumu lolote lililopewa chini ya Sheria hii.

(2) Baraza linaweza, wakati wa utekelezaji wa kazi zake, kushirikiana na taasisi au mamlaka nyengine zinazofanana juu ya mambo yanayohusiana na mafunzo na utendaji wa Waatalamu wa Maabara ya Tiba.

Uwezo wa Baraza.

**6.** Uwezo wa Baraza utakuwa ni:

(a) kumtahadharisha, kumsitisha na kumuondosha katika utendaji wa kazi za Maabara, mtaalamu yeyote wa Maabara ya Tiba ikiwa ameenda kinyume na masharti ya Sheria hii;

(b) kutoza ada kwa ajili ya huduma inayotolewa na Baraza kama inavyohitajika na masharti ya Sheria hii; na

(c) kuidhinisha au kutoidhinisha bajeti ya mwaka.

Kukasimu uwezo na kazi za Baraza.

7.-(1) Baraza linaweza, kwa kuzingatia masharti, taratibu na mipaka, kama itakavyoweza kuainisha, kukasimu kwa maandishi kwa Kamati yoyote au Mrajis wa Baraza baadhi ya kazi, uwezo au majukumu iliyopewa chini ya Sheria hii.

(2) Kukasimu kulikofanywa chini ya kifungu hiki hakutozuia Baraza kutenda au kutekeleza kazi, uwezo au majukumu yaliyokasimiwa.

(3) Bila ya kujali masharti ya vifungu vidogo vya (1) na (2) vya kifungu hiki, Baraza halitokuwa na uwezo wa kukasimu:

(a) uwezo wa kuidhinisha au kutoidhinisha bajeti ya mwaka; na

(b) uwezo wa kuidhinisha au kubadilisha maeneo ya mafunzo, mitaala na viwango vyengine vinavyohusiana na taaluma za wataalamu wa maabara Zanzibar.

Kamati za Baraza.

**8.**-(1) Baraza linaweza, kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa kazi zake, kuanzisha Kamati zifuatazo:

(a) Kamati ya Mafunzo, Utafiti na Taaluma;

(b) Kamati ya Uhakiki wa Viwango vya Ubora;

(c) Kamati ya Maadili na Miiko; na

(d) Kamati ya Sera, Mipango na Fedha.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Baraza linaweza kuanzisha kamati nyengine yoyote kutekeleza kazi maalum kama itakavyoona inafaa.

Kazi za Kamati.

**9.**-(1) Kazi za Kamati ya Mafunzo, Utafiti na Taaluma zitakuwa:

(a) kushauri kuhusiana na mitihani inayotolewa kwa Wataalamu wa Maabara za Tiba kabla ya usajili;

(b) kupitia mitaala ya mafunzo kwa Wataalamu wa Maabara ya Tiba;

(c) kufanya ukaguzi wa programu za mafunzo kwa ajili ya kuangalia kiwango cha elimu kinachotolewa na kulishauri Baraza katika maeneo ya kuendelezwa;

(d) kulishauri Baraza juu ya mambo yote yanayohusiana na utafiti katika taaluma ya Maabara ya Tiba;

(e) kukuza na kuendeleza utaalamu wa Waatalam wa Maabara ya Tiba katika njia za utafiti kwa kushirikiana na taasisi za afya za utafiti na watafiti wengine ndani na nje ya Zanzibar;

(f) kuainisha na kuzitathmini sifa za usajili, kuingiza jina katika Daftari na utoaji wa leseni, na kutoa mapendekezo kwa Baraza;

(g) kutoa miongozo kwa Wataalam wa Maabara ya Tiba kuhusu mambo ya elimu na mafunzo endelevu ya sayansi ya maabara ya tiba kupitia machapisho, semina na mikutano;

(h) kuanzisha viwango vya chini vya utendaji vya taaluma ya Maabara ya Tiba; na

(i) kutekeleza kazi nyengine yoyote kama itakavyopewa na Baraza.

(2) Kazi za Kamati ya Uhakiki wa Viwango vya Ubora zitakuwa:

(a) kuendeleza programu za uhakiki wa viwango vya ubora na kufanya marekebisho ya programu hizo kama inavyohitajika;

(b) kulishauri Baraza juu ya mambo yote yanayohusiana na utoaji wa huduma bora za maabara;

(c) kuendeleza miongozo ya kisera na uratibu kwa ajili ya matumizi ya Wataalam wa Maabara ya Tiba na wafanyakazi wengine wa huduma ya afya katika kusimamia programu za uhakiki wa viwango vya ubora;

(d) kuweka masharti na viwango vya Maabara za Tiba;

(e) kuhakikisha kwamba huduma bora za maabara, viwango vya ujuzi, taaluma na umahiri wa Wataalamu wa Maabara ya Tiba zinaimarishwa na kuhifadhiwa;

(f) kuhakikisha Wataalamu wa Maabara ya Tiba wanafuata Sheria ya Wataalamu wa Maabara za Tiba na Kanuni; na

(g) kutekeleza kazi nyengine yoyote itakayopewa na Baraza.

(3) Kazi za Kamati ya Maadili na Miiko zitakuwa ni:

(a) kulishauri Baraza juu ya maadili na miiko katika utaalamu wa Maabara ya Tiba;

(b) kupitia malalamiko ya ukiukaji wa maadili ya kitaaluma yanayowasilishwa kwa Baraza na kutoa mapendekezo juu ya hatua muafaka itakayochukuliwa dhidi ya mtuhumiwa; na

(c) kutekeleza kazi nyengine yoyote itakayopewa na Baraza.

(4) Kazi za Kamati ya Sera, Mipango na Fedha zitakuwa ni:

(a) kusaidia juu ya uendelezaji wa mpango mkakati wa Baraza;

(b) kusaidia Baraza juu ya uendelezaji wa Miongozo ya Sera na taratibu;

(c) kuandaa makisio ya bajeti ya mwaka ya Baraza;

(d) kupitia taarifa za ukaguzi wa fedha kabla hazijawasilishwa katika Baraza;

(e) kulishauri Baraza juu ya masuala ya kifedha; na

(f) kutekeleza kazi nyengine yoyote kama itakavyopewa na Baraza.

Muundo wa Kamati.

**10.** Muundo, utaratibu na masharti na mipaka mengine ya Kamati ni kama itakavyoelezwa na Baraza.

## SEHEMU YA TATU
## UENDESHAJI NA WAFANYAKAZI WA BARAZA

Uteuzi wa Mrajis.

**11.**-(1) Kutakuwa na Mrajis wa Baraza atakayeteuliwa na Rais.

(2) Mrajis atakuwa ni Afisa Mtendaji Mkuu wa Baraza na atakuwa na wajibu wa kuongoza na kusimamia kazi za Baraza.

Sifa za Mrajis.

**12.** Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mrajis, ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza ya sayansi za Maabara ya Tiba;

(c) ni mtaalam mwandamizi wa Maabara ya Tiba kutoka katika utumishi wa umma na ana uzoefu wa kazi angalau wa miaka kumi katika fani hiyo; na

(d) ana uadilifu wa hali ya juu.

Kazi za Mrajis.

**13.**-(1) Kazi za Mrajis zitakuwa ni:

(a) kusajili Wataalamu wa Maabara ya Tiba baada ya kuidhinishwa na Baraza;

(b) kuweka na kuhifadhi Daftari na kumbukumbu zote za Wataalamu wa Maabara ya Tiba waliosajiliwa;

(c) kufanya mabadiliko muhimu, kusahihisha na kuondosha taarifa zozote zilizomo katika Daftari kama atakavyoelekezwa na Baraza;

(d) kwa kushirikiana na Wakaguzi wa Maabara za Tiba, kuwa na fursa kamili, kwa niaba ya Baraza, kukagua mambo yanayohusiana na huduma za kimaabara ya tiba;

(e) kurekodi na kuzihifadhi kumbukumbu na taratibu za mikutano ya Baraza na Kamati zake;

(f) kupokea malalamiko na kuwasilisha katika Baraza;

(g) kuwa mtunzaji wa muhuri wa Baraza;

(h) kuwa na wajibu wa usimamizi wa fedha, mali, watumishi na rasilimali nyengine zozote za Baraza;

(i) kuendeleza na kutekeleza sera na mipango ya Baraza;

(j) kuwa ni mamlaka ya nidhamu kwa watumishi wa Baraza; na

(k) kutekeleza kazi nyengine zozote kama atakavyoelekezwa na Baraza kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii.

(2) Mrajis, katika kutekeleza kazi zake atawajibika kwa Baraza;

Uteuzi, sifa na kazi za Naibu Mrajis.

**14.**-(1) Kunaweza kuwa na Naibu Mrajis atakayeteuliwa na Rais.

(2) Sifa za Naibu Mrajis zitakuwa sawa na sifa za Mrajis.

(3) Naibu Mrajis atafanya kazi ya kumsaidia Mrajis katika kazi za kila siku za Baraza na atatekeleza kazi nyengine kama zitakavyoelezwa na Baraza.

Daftari na machapisho.

**15.**-(1)Baraza litaanzisha Daftari kwa ajili ya Wataalamu wa Maabara za Tiba ambalo litawekwa na kuhifadhiwa na Mrajis.

(2) Daftari litakuwa na namba ya usajili, jina, anuani, sifa na taarifa nyengine za Wataalamu wote wa Maabara za Tiba ambao wana sifa za kusajiliwa.

(3) Mrajis atakuwa:

(a) ni mtunzaji wa Daftari; na

(b) ana dhamana ya kuhifadhi na kuingiza upya taarifa katika Daftari kama atakavyoelekezwa na Baraza.

(4) Mrajis atachapisha katika Gazeti Rasmi la Serikali katika kila mwaka, orodha ya majina ya Wataalamu wa Maabara za Tiba waliosajiliwa.

Maafisa na watumishi wa Baraza.

**16.**-(1) Kutakuwa na watumishi wa Baraza watakaoajiriwa kulingana na masharti na taratibu kwa mujibu wa masharti yao ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.

(2) Maafisa na Sekretarieti ya Baraza, wakati wa utekelezaji wa kazi zao, watawajibika kwa Mrajis.

## SEHEMU YA NNE
## USAJILI NA LESENI

Maombi ya usajili na kupata leseni.

**17.**-(1) Mtu ambaye ana sifa za kufanya kazi za Maabara ya Tiba ndani ya Zanzibar ataomba katika Baraza kusajiliwa na kupata leseni.

(2) Baraza litapitia maombi yaliyofanywa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki na litamsajili muombaji aliyetimiza masharti yaliyoainishwa katika Sheria hii na Kanuni zake.

(3) Ombi hilo litaamuliwa ndani ya siku thelathini za kazi kutoka tarehe ya kuwasilishwa ombi hilo.

(4) Ikitokezea ombi halijaamuliwa ndani ya muda ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, Mrajis atawasiliana au kumpa sababu muombaji za kushindwa kufanya hivyo.

(5) Baraza, baada ya malipo ya ada iliyoainishwa na baada ya kuridhika kwamba muombaji amekidhi masharti yaliyotakiwa kumuwezesha kufanya kazi kama Mtaalamu wa Maabara ya Tiba, litampa leseni ya kufanya kazi katika fani hiyo.

(6) Baraza linaweza kukataa ombi lolote lililofanywa chini ya kifungu hiki, isipokuwa kwamba Baraza litampa taarifa muombaji sababu za kukataa huko.

(7) Baraza halitomsajili na kutoa leseni kwa mtu yeyote ambaye ameondolewa katika daftari la nchi nyengine yoyote.

(8) Mtu yeyote ambae hakuridhika na uamuzi wa Baraza chini ya Sehemu hii anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi huo kwa Waziri.

Sifa za usajili.

**18.**-(1) Kwa kuzingatia mashari ya Sheria hii, mtu yeyote atakuwa na sifa za kusajiliwa kama Mtaalamu wa Maabara ya Tiba baada ya kukidhi masharti yafuatayo:

(a) amekamilisha kwa ukamilifu mafunzo kama Mtaalamu wa Maabara ya Tiba na akatunukiwa stashahada, stashahada ya juu, shahada ya kwanza au zaidi kutoka katika chuo kinachotambulika;

(b) awe na vyeti vya taaluma vilivyotolewa na taasisi inayotambulika; na

(c) awe na ushahidi wa kukamilisha mafunzo ya vitendo kwa angalau mwenye shahada ya kwanza;

(2) Kwa mtu ambaye sio mkaazi wa Zanzibar:

(a) atawasilisha ushahidi wa kuiridhisha Baraza kwamba amesajiliwa au kwamba alisajiliwa na bado anastahiki kusajiliwa kama Mtaalamu wa Maaabara ya Tiba katika nchi aliyotoka;

(b) atawasilisha ushahidi kuwa amekamilisha kikamilifu mafunzo kama Mtaalamu wa Maabara ya Tiba katika taasisi inayotambulika na Baraza;

(c) atatakiwa kuwa na cheti au hati ya utambulisho iliyotolewa na nchi aliyofanya kazi mwisho; na

(d) awe na hati halali ya kusafiria.

(3) Endapo kumekosekana ushahidi ulioainishwa katika kifungu kidogo cha (2)(a) na (b) cha kifungu hiki, Baraza litamfanyia mtihani mtu ambaye anayeomba usajili, na mtu huyo atatakiwa kufaulu mtihani huo.

(4) Bila ya kuathiri ujumla wa masharti chini ya vifungu vidogo vya (1), (2) na (3) vya kifungu hiki, ombi hilo litaambatanishwa na nakla za nyaraka zilizothibitishwa zifuatazo:

(a) risiti ya ada ya usajili na leseni;

(b) wasifu binafsi;

(c) picha mbili ndogo za paspoti zilizopigwa karibuni; na

(d) masharti mengine ya ziada na ushahidi unaohusiana na kupata uzoefu wa kazi katika Maabara ya Tiba kama Baraza litakavyoeleza,

Usajili wa mpito.

**19.**-(1) Mtu yeyote ambaye hana sifa za kusajiliwa kama Mtaalamu wa Maabara ya Tiba baada ya kukamilisha mafunzo, ikiwa atawasilisha ushahidi utakaoridhisha Baraza kwamba amechaguliwa kufanya mafunzo ya vitendo katika hospitali inayotambulika na Baraza kwa madhumuni ya kifungu hiki na kwamba mafunzo hayo yanatoa uzoefu unaotakiwa, atastahiki kupewa usajili wa mpito.

(2) Mtaalamu wa Maabara ya Tiba aliyesajiliwa kwa masharti ya mpito, pale itakapoonekana inafaa, atawezeshwa kupata uzoefu wa vitendo kwa madhumuni yalioainishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(3) Mtu ambaye amepata usajili wa mpito baada ya malipo ya ada iliyoainishwa, atapewa cheti cha usajili wa mpito.

Usajili wa Muda.

**20.**-(1) Endapo mtuataliridhisha Baraza kuwa:

(a) sio Mtanzania au mkaazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(b) ameajiriwa au anakusudia kuajiriwa Zanzibar kwa nafasi yake ya kwamba anaomba kwa madhumuni ya kutekeleza kazi maalumu ya utafiti na ufundishaji;

(c) anaingia au kabla hajaingia Zanzibar alikuwa katika kazi kama Mtaalam wa Maabara ya Tiba; na

(d) atafuata masharti ya Sheria hii na Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii,

Baraza linaweza kumsajili mtu huyo kwa kipindi kilichoainishwa kwa kazi maalumu au kipindi ambacho Baraza linaweza kuamua, kwa namna yoyote ile, lakini kipindi hicho hakitazidi miezi sita.

(2) Kwa madhumuni ya kukidhi masharti chini ya kifungu cha 18 cha Sheria hii, Baraza linaweza kutoa maelekezo kwa mtu ambae sio mkaazi wa Zanzibar kufanya mtihani baada ya kulipa ada iliyoainishwa.

Mtu aliyesajiliwa kufanya kazi kwa mujibu wa maadili na miiko ya utendaji.

**21.**-(1) Mtaalam wa Maabara ya Tiba aliyesajiliwa, atawahudumia wagonjwa kwa mujibu wa maadili ya kimaabara na miiko ya utendaji iliyowekwa chini ya Sheria hii.

(2) Mtaalam wa Maabara ya Tiba aliyesajiliwa atafuata masharti ya uhakiki wa ubora ikijumuisha udhibiti wa ubora wa ndani na atashiriki tathmini ya utendaji wa ubora wa nje pale itakapohitajika.

Ukaguzi wa programu za mafunzo ya Maabara ya Tiba.

**22.** Mrajis, kwa kushirikiana na Mkaguzi au mtu mwengine yeyote aliyeidhinishwa na Baraza, anaweza kwa madhumuni ya kuhakikisha masharti ya Sheria hii yanafuatwa, kuingia na kukagua taasisi yoyote inayotoa programu za mafunzo ya Maabara ya Tiba.

Uteuzi, kazi na uwezo wa Mkaguzi wa Maabara ya Tiba.

**23.**-(1) Baraza litateua mtu miongoni mwa Wataalamu wa Maabara ya Tiba kuwa Mkaguzi.

(2) Mkaguzi aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atatekeleza kazi zifuatazo:

(a) kwa wakati wote muafaka, anaweza kuingia katika Maabara za Tiba za umma au za binafsi kwa ajili ya ukaguzi kuhusiana na mambo yanayosimamiwa chini ya Sheria hii;

(b) kwa kushirikiana na Mamlaka husika, anaweza kuisimamisha kwa muda Maabara ya Tiba yoyote iliyoonekana inaenda kinyume na masharti ya Sheria hii; na

(c) atafanya au atatekeleza kazi nyengine zozote kama atakavyopewa na Mrajis au Baraza kwa mujibu wa Sheria hii.

(3) Baada ya ukaguzi, Mkaguzi wa Maabara ya Tiba, ndani ya kipindi cha wiki mbili, atawasilisha taarifa kwa Baraza.

Mkaguzi wa Maabara ya Tiba atapewa Kitambulisho.

**24.**-(1) Kila Mkaguzi atapewa kitambulisho na Baraza.

(2) Mkaguzi atachukua kitambulisho muda wote ambao anatekeleza kazi na uwezo wake kwa mujibu wa Sheria hii.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA NIDHAMU

Mrajis kupokea malalamiko.

**25.**-(1) Mrajis, kwa niaba ya Baraza, atapokea malalamiko kutoka kwa mtu yeyote dhidi ya Mtaalamu wa Maabara ya Tiba au kituo cha afya kinachokwenda kinyume na atayawasilisha malalamiko hayo kwa Baraza.

(2) Baraza linaweza kuzingatia kuwa Mtaalamu wa Maabara ya Tiba hafai kufanya kazi.

(3) Kwa madhumuni ya kifungu hiki, "kutofaa kufanya kazi" maana yake ni mtu ambae kufaa kwake kufanya kazi kumezorota kwa sababu ya:

(a) kwenda kinyume na maadili ya kitaaluma dhidi ya maadili na miiko ya utendaji wa Maabara ya Tiba;

(b) kukosekana kwa umahiri;

(c) kuzorota afya yake ya kimwili na kiakili;

(d) uamuzi wa Bodi ya Madaktari inayotambulika au bodi nyengine yoyote iliyoidhinishwa kushughulika na afya; au

(e) taratibu za mamlaka nyengine yoyote.

(4) Kwa madhumuni ya masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, maneno "makosa ya kimaadili" yanajumuisha:

(a) kwenda kinyume na sharti lolote la Sheria hii au Kanuni zake;

(b) kushindwa kufuata taratibu, masharti au mipaka ya leseni kama Mtaalamu wa Maabara ya Tiba aliyesajiliwa;

(c) kumuathiri mgonjwa kimaneno, kivitendo, kijinsia au kiakili;

(d) kuwa na mgongano wa maslahi ambao unaathiri uhusiano baina ya mgonjwa na mtaalamu;

(e) kumshawishi mgonjwa kubadilisha matakwa yake, tiba sahihi au miongozo ya hati ya uwakala;

(f) kumtelekeza mgonjwa ambae anahitaji uangalizi;

(g) kufanya uchunguzi usio sahihi;

(h) kushindwa kutoa taarifa ya kutokuwa na umahiri, uzembe au kwenda kinyume na maadili kuhusu mtendaji ambae utendaji wake unahatarisha afya ya mgonjwa;

(i) kushindwa kutumia nafasi yake kuhusiana na kuvujisha taarifa za siri zinazomuhusu mgonjwa;

(j) kutoa taarifa za uongo kuhusiana na uchunguzi wa mtokeo ya mgonjwa;

(k) kushindwa kutimiza viwango vya utendaji kazi na maadili na miiko ya taaluma; na

(l) utendaji wowote au kitendo chochote kinachohusiana na utoaji huduma ambacho kinazingatia mazingira yote yanayotakiwa kuzingatiwa katika taaluma kama kutokuheshimiwa, kwenda kinyume na maadili ya taaluma au kuathiri huduma kwa mgonjwa.

(5) Kila lalamiko chini ya kifungu hiki litaambatana na maelezo ya maandishi yaliyoandaliwa na mlalamikaji, au mtu yeyote kwa niaba ya mlalamikaji au mtu yeyote mwenye maslahi katika kutenda au kutokutenda kunakopelekea lalamiko.

(6) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (5) cha kifungu hiki, Baraza linaweza lenyewe kufanya uchunguzi wowote wa awali kuhusiana na mtaalamu wa Maabara ya Tiba ikiwa imejiridhisha kwamba taarifa iliyopokelewa na Baraza inahitaji kufanyika uchunguzi wa awali.

Uchunguzi wa Baraza.

**26.** Baraza linaweza kufanya uchunguzi dhidi ya Mtaalam wa Maabara ya Tiba aliyesajiliwa ikiwa mtu huyo:

(a) ametuhumiwa kwa kosa chini ya Sheria hii;

(b) ametuhumiwa kwa kosa la jinai linalohusisha kukosa uaminifu au udanganyifu au kwenda kinyume na maadili; au

(c) ametuhumiwa kutenda kosa kinyume na utendaji, uzembe au kinyume na maadili ya taaluma au kutokufuata kanuni yoyote au maelekezo yaliyotolewa chini ya Sheria hii.

Uwezo wa Baraza wa kuchukua hatua za kinidhamu.

**27.**-(1) Mrajis, baada ya kupokea malalamiko dhidi ya Mtaalamu wa Maabara ya Tiba, anaweza, ndani ya siku thelathini, kumsimamisha Mtaalamu wa Maabara ya Tiba kwa muda maalum hadi utakapokamilika uchunguzi wa Baraza.

(2) Baraza lina uwezo wa kukusanya ushahidi na kutaka kutolewa nyaraka zozote kwa ajili ya uchunguzi unaofanywa chini ya Sheria hii.

(3) Baada ya uchunguzi kukamilika kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Baraza linaweza:

(a) kusimamisha, kuthibitisha, kuongeza au kupunguza muda maalumu wa kusimamisha; au

(b) kutoa amri ya:

(i) kuliondosha jina la Mtaalamu wa Maabara ya Tiba kutoka katika Daftari;

(ii) kumsimamisha Mtaalamu wa Maabara ya Tiba kufanya kazi kwa kipindi ambacho litaona inafaa; au

(iii) kumuonya, kumkaripia au vyenginevyo kumpa karipio kali Mtaalamu wa Maabara ya Tiba.

(4) Adhabu, isiyokuwa ya kusimamisha kwa muda au kwa muda maalumu, haitaweza kutolewa kwa Mtaalamu wa Maabara ya Tiba isipokuwa uchunguzi uwe umefanywa.

(5) Ndani ya siku saba za kazi baada ya kukamilisha uchunguzi, Mrajis atawasilisha uamuzi wa Baraza kwa wahusika.

Kudharau wito na kukataa kutoa ushahidi.

**28.**-(1) Mtu yeyote ambaye amepewa wito wa kuhudhuria au kutoa ushahidi au kuwasilisha nyaraka yoyote kwa ajili ya uchunguzi wowote unaofanywa chini ya Sheria hii:

(a) kashindwa bila ya sababu ya msingi kuitikia wito;

(b) kakataa bila ya sababu ya msingi kujibu maswali aliyoulizwa na Baraza; au

(c) kwa makusudi anaingilia mwenendo wa Baraza au anamkejeli mjumbe wa Baraza,

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Tano za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi miwili au adhabu zote mbili.

(2) Mtu yeyote ambaye atatoa ushahidi mbele ya Baraza kwa madhumuni ya ushahidi aliyoutoa au waraka mwengine wowote aliyoutoa, atastahiki kupata fursa zote ambazo angestahiki kupewa kama shahidi mbele ya mahakama.

Kuondolewa katika Daftari.

**29.**-(1) Baraza linaweza kuondoa kutoka katika Daftari jina la mtu yeyote aliyesajiliwa ambaye anashindwa kufuata masharti ya Sheria hii.

(2) Mtu yeyote ambaye jina lake limeondolewa kutoka katika Daftari hatoajiriwa au kufanya kazi kama Mtaalamu wa Maabara ya Tiba ndani ya Zanzibar.

(3) Baraza litatangaza jina la Mtaalamu wa Maabara ya Tiba aliyeondolewa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Kuwasilisha cheti kuhusiana na kuondolewa jina kutoka katika Daftari.

**30.**-(1) Mtu yeyote ambaye jina lake limetakiwa kuondolewa kutoka katika Daftari chini ya masharti ya Sheria hii, ndani ya siku thelathini tokea kupewa taarifa ya amri hiyo au kuondolewa rufaa yoyote dhidi ya amri hiyo, kwa mujibu wa sheria, atawasilisha kwa Baraza cheti au leseni yoyote iliyotolewa kwake na Baraza.

(2) Mtu yeyote ambaye anashindwa kufuata masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua

Shilingi Laki Tano za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita na Mahakama itatoa amri kwamba cheti hicho kifutwe.

Rufaa dhidi ya kusimamisha utendaji au kuondosha kutoka katika Daftari

**31.** Mtu yeyote ambaye anahisi hakuridhika na amri yoyote au uamuzi wa Baraza anaweza kukata rufaa kwa Waziri dhidi ya amri au uamuzi huo.

Kulirejesha jina baada ya kuondolewa.

**32.** Baraza linaweza, baaada ya maombi ya mtu ambaye jina lake limeondolewa kutoka katika Daftari, na baada ya kukamilika kipindi kilichoelezwa, kulirejesha jina la mtu huyo baada ya malipo ya ada iliyoelezwa na kukidhi masharti mengine yaliyoelezwa.

Masharti ya kurejesha jina katika Daftari.

**33.**-(1) Baraza litarejesha jina la mtu katika Daftari kumuwezesha kufanya kazi ikiwa mtu huyo amekidhi masharti yafuatayo:

(a) alisimamishwa kufanya kazi kwa kipindi cha miaka miwili na maombi yake yakasikilizwa na Baraza na kuthibitishwa kuwa anafaa kufanya kazi ya teknolojia ya Maabara ya Tiba;

(b) amethibitika kwamba siyo mkosa wa kosa alilotuhumiwa nalo kuwa amelifanya; na

(c) amethibitika kuwa hana hatia baada ya kufuata masharti yaliyowekwa na Baraza.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Baraza linaweza kutoa masharti mengine ya kufuatwa baada ya kuainisha jina la kosa au kwenda kinyume kwa muombaji.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA FEDHA

Vyanzo vya fedha vya Baraza.

**34**-(1) Vyanzo vya fedha na rasilimali za Baraza vitajumuisha:

(a) fedha kama zitakavyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi;

(b) ada au tozo zinazopokelewa na Baraza kutokana na utekelezaji wa kazi zake;

(c) michango halali, misaada, urithi au mikopo inayoweza kupokelewa kutoka kwa mtu yeyote au taasisi; na

(d) fedha nyengine zozote zitakazopatikana na Baraza.

(2) Matumizi yote ya Baraza yatafanywa kutoka katika fedha za Baraza kama yatakavyothibitishwa na Baraza.

Hesabu na Ukaguzi.

**35.**-(1) Mrajis ataweka na kuhifadhi ipasavyo vitabu vya hesabu ambavyo vitajumuisha kumbukumbu zote za fedha na miamala kwa kila mwaka wa fedha.

(2) Kumbukumbu za fedha za Baraza zitakaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kutumika kwa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma.

**36.** Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na sheria nyengine zinazohusiana na fedha za umma zitatumika katika miamala na mambo yote ya fedha za Baraza, ikijumuisha:

(a) makadirio ya mwaka;

(b) makadirio ya fedha za ziada;

(c) uwekaji na uhifadhi wa vitabu vya hesabu;

(d) uandaaji wa taarifa za fedha;

(e) ukaguzi na hesabu; na

(f) miamala mengine yoyote ya Baraza.

Ripoti ya Mwaka.

**37.**-(1) Baraza, ndani ya miezi sita baada ya mwisho wa kila mwaka wa fedha, litawasilisha kwa Waziri ripoti ya mwaka katika mwaka huo wa fedha ikijumuisha:

(a) nakala ya hesabu zilizokaguliwa za Baraza, pamoja na ripoti ya mkaguzi kuhusiana na hesabu hizo;

(b) ripoti ya utekelezaji wa Baraza katika kipindi cha mwaka wa fedha huo; na

(c) taarifa nyengine zozote zinazohusiana na kazi za Baraza kama Waziri atakavyohitaji.

(2) Mwaka wa fedha unaanza kutoka tarehe 1 Julai hadi tarehe 30 Juni ya mwaka unaofuata.

## SEHEMU YA SABA
## MAKOSA NA ADHABU

Kufanya kazi kinyume na Sheria.

**38.**-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) anafanya kazi ya teknolojia ya maabara bila ya usajili na leseni halali;

(b) amesimamishwa kufanya kazi kama Mtaalamu wa Maabara ya Tiba kwa amri ya Baraza, kwa tabia zake au kwa ajili ya kujinufaisha anafanya kazi kama Mtaalamu wa Maabara ya Tiba;

(c) ameondolewa kutoka katika Daftari; au

(d) ameshindwa kutekeleza amri au maelekezo ya Baraza.

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili.

(2) Endapo mtu anatiwa hatiani kwa kosa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Mahakama inaweza kutoa amri ya kifaa chochote au vitu vilivyotumika vikiwa ni mali au vimeonekana vipo katika umiliki wa mtu aliyetiwa hatiani, kuwa vichukuliwe, vitaifishwe au vinginevyo viteketezwe.

Taarifa au nyaraka za udanganyifu.

**39.** Mtu yeyote ambaye:

(a) anapata au anajaribu kupata usajili au leseni kwa njia ya kufanya au anasababisha kufanyika au kutoa taarifa au nyaraka za undanganyifu au uongo;

(b) kwa makusudi anafanya au anasababisha kufanyika udanganyifu wowote katika jambo lolote linalohusiana na Daftari; au

(c) anasaidia kwamba mtu huyo kuingizwa katika Daftari,

atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili za Kitanzania au kifungo kwa kipindi cha miaka mitatu au adhabu zote mbili.

Kuanzisha programu ya teknolojia ya maabara ya tiba.

**40.** Taasisi yoyote inayoanzisha skuli ya mafunzo ya teknolojia ya Maabara ya Tiba au inakusudia kutoa mafunzo ya kada yoyote ya Maabara ya Tiba bila ya idhini ya Baraza, itakuwa imetenda kosa na itakapotiwa hatiani, italipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Nne za Kitanzania na lakini isiyozidi Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania.

Kujifananisha na kupotosha.

**41.** Mtu ambaye anajifananisha, anapotosha, anajinasibisha na anatumia majina, vyeo na sare za Mtaalamu wa Maabara ya Tiba aliyesajiliwa, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili za Kitanzania au kifungo kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili.

Masharti yanayohusiana na utaratibu wa Baraza.

**42.** Mtu yeyote ambaye anakwenda kinyume na kifungu cha 28 cha Sheria hii, atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili.

Kumuajiri mtu asiyesajiliwa au kupewa leseni.

**43.** Mtu ambaye anamuajiri mtu yeyote kufanya kazi ya teknolojia ya Maabara ya Tiba kama Mtaalamu wa Maabara ya Tiba aliyesajiliwa ambaye hakusajiliwa au kupewa leseni, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka miwili au adhabu zote mbili.

Kusaidia kutenda kosa.

**44.** Mtu ambaye anamsaidia mtu mwingine kutenda kosa chini ya Sheria hii, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja na Laki Tano za Kitanzania au kifungo kisichozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili.

Adhabu kwa kumzuia au kumlazimisha Mkaguzi.

**45.** Mtu yeyote ambaye kwa makusudi anamzuia kwa njia yoyote ile au anamlazimisha Mkaguzi, Mrajis au Afisa yeyote aliyeidhinishwa na Baraza kufanya ukaguzi au kutumia uwezo wake, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu au adhabu zote mbili.

Machapisho.

**46.**-(1) Mtu yeyote ambaye anachapisha au katika namna yoyote ile, anatoa taarifa kwa umma au anasababisha au anaruhusu kuchapishwa udanganyifu wowote au matangazo ya aina yoyote yanayopotosha huduma za aina yoyote za Maabara ya Tiba au mafunzo ya maabara, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au kifungo kisichozidi miezi sita.

(2) Mtu ambaye anachapisha au anatangaza huduma za Maabara ya Tiba, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichozidi miezi sita au adhabu zote mbili.

Adhabu za ujumla.

**47.** Mtu ambaye anatenda kosa chini ya Sheria hii ambalo adhabu yake maalumu haikutajwa na baada ya kutiwa hatiani, atalipa faini isiyopungua Shilingi Laki Sita za Kitanzania au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita au adhabu zote mbili.

## SEHEMU YA NANE
## MASHARTI MENGINEYO

Ada na tozo.

**48**. Kutakuwa na kiwango cha ada na tozo kitakacholipwa kwa Baraza kwa huduma zinazotolewa na Baraza, kwa kiwango kitakachoainishwa na Waziri kila baada ya muda.

Mtaalamu wa Maabara ya Tiba aliyesajiliwa kutoa huduma bora za maabara za tiba.

**49**.-(1) Mtaalamu wa Maabara aliyesajiliwa atatoa huduma za Maabara ya Tiba kwa kuzingatia:

(a) Maadili na Miiko ya Maabara za Tiba;

(b) Mfumo wa Usimamizi wa Ubora, Viwango vya Maabara ya Tiba vya Kitaifa na Kimataifa; na

(c) taaluma yenye uweledi, uadilifu na uaminifu na kuwasiliana ipasavyo pamoja na kuonesha mienendo mizuri kwa wagonjwa na wataalamu wenzake.

(2) Mtaalamu wa Maabara ya Tiba aliyesajiliwa:

(a) atalinda ustawi wa wagonjwa na kuheshimu utu wa kila mmoja;

(b) atakaa nao vizuri wagonjwa, watumiaji huduma na watumishi kwa kiwango kilicho sawa cha heshima bila ya kuwabagua kwa msingi wa jinsia, dini, kabila, ulemavu au umri;

(c) atakuza taswira na hadhi ya taaluma zao kwa kuhifadhi viwango vya juu katika utendaji wa taaluma zao na kwa msaada wa taasisi zao za kitaaluma;

(d) hatafuata taratibu ambazo, binafsi, anaamini sio za kimaadili, si za kisheria au zinaweza kuwaletea madhara wagonjwa;

(e) atafanya kazi ndani ya mipaka yao ya kimaadili ya taaluma;

(f) atafuata masharti ya taaluma hii na masharti ya Sheria hii na Kanuni zake;

(g) atahifadhi siri za taarifa zote za mgonjwa kwa mujibu wa Sheria iliyopo;

(h) atatekeleza majukumu yote kwa kufuata sheria za nchi kwa ajili ya kuwalinda wagonjwa, watoa huduma ya afya, wananchi kwa jumla na mazingira;

(i) atatoa taarifa kwa muhusika kama kuna jambo linaingilia uwezo wake wa kutekeleza majukumu kwa ufanisi;

(j) atazingatia majukumu ya kitaaluma kwa ajili ya utekelezaji na kufuata viwango vya utendaji na mifumo ya ubora;

(k) atatatua migongano ya kimaslahi ya kimaabara za tiba kwa kulinda maslahi ya mgonjwa au watumiaji wa huduma ya maabara;

(l) atatumia zana na vifaa vya maabara kwa usahihi na hatapoteza vitendanishi au vifaa vyengine vya maabara;

(m) ataonesha na atafuata taratibu na kanuni za kiusalama na za kiulinzi za maabara;

(n) hatatekeleza au hatapendekeza taratibu za uchunguzi wa maabara ambazo sio muhimu au zitaigharimu utoaji wa huduma wa maabara katika njia ya udanganyifu au upotoshaji;

(o) hatokasimu kwa mtu asiye na sifa ya Mtaalamu wa Maabara ya Tiba kufanya kazi ya Maabara ya Tiba; na

(p) atabadilishana utaalamu na wataalamu wenziwe na atashirikiana kikamilifu na wataalamu wengine wa afya katika kutoa huduma bora za maabara na uangalizi.

(3) Mtu ambaye anakwenda kinyume na masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa.

Kanuni.

**50.**-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni za kijumla kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Waziri anaweza kutunga Kanuni zinazoelezea:

(a) ada na tozo zitakazolipwa chini ya Sheria hii, ikijumuisha ada inayolipwa kwa ajili ya usajili chini ya Sheria hii;

(b) viwango na masharti ya utendaji kazi za kitaaluma kwa Wataalamu wa Maabara ya Tiba;

(c) maadili na miiko kwa Wataalamu wa Maabara ya Tiba;

(d) fomu za maombi, utaratibu na masharti mengineyo kwa ajili ya usajili wa mtu chini ya Sheria hii;

(e) mitihani ambayo inaweza kufanywa kwa mujibu wa Sheria hii;

(f) ukaguzi wa Maabara za Tiba;

(g) taarifa zinazohitajika kutolewa kupitia notisi chini ya Sheria hii;

(h) usimamizi na udhibiti wa jambo lolote kuhusiana na utendaji kazi wa huduma za kimaabara;

(i) taratibu zinazohusiana na mchakato wowote au mienendo chini ya Sheria hii;

(j) taratibu za kukata rufaa au kufanya uchunguzi; na

(k) orodha ya nchi zenye sifa za kutoa leseni kwa Wataalamu wa Maabara za Tiba.

## JADWELI

## MASHARTI YANAYOHUSIANA NA UENDESHAJI WA MIKUTANO YA BARAZA

**[Chini ya kifungu cha 4(8)**

*Mikutano ya Baraza.*

**1.**-(1) Baraza litakutana kikawaida kila baada ya miezi mitatu au linaweza kukutana wakati wowote pale inapohitajika kwa ajili ya kutekeleza kazi katika pahala ambapo Baraza linaweza kuainisha kila baada ya muda.

(2) Mikutano yote ya Baraza itaongozwa na Mwenyekiti au endapo hayupo, wajumbe waliohudhuria watamchagua mmoja miongoni mwao kuendesha mkutano na mjumbe aliyechaguliwa atatumia uwezo na atatekeleza majukumu yote ya Mwenyekiti.

*Akidi ya Mkutano*

**2.** Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe watatimiza akidi ya mkutano wowote wa Baraza.

*Maamuzi ya Baraza*

**3.**-(1) Baraza litafanya maamuzi yake kwa makubaliano ya wajumbe wote na endapo hakuna makubaliano, uamuzi utafikiwa kwa kura na endapo kura ziko sawa, Mwenyekiti au Mjumbe anayeongoza mkutano atakuwa na kura ya maamuzi.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, maamuzi yanaweza kufanywa na Baraza kwa kusambaza nyaraka kwa wajumbe ili kila mjumbe aeleze maoni yake kwa maandishi isipokuwa kwamba mjumbe yeyote anaweza kutaka uamuzi huo kuletwa katika mjadala katika mkutano wa Baraza.

(3) Maamuzi yatakayopatikana kwa maoni ya kila mjumbe yatakuwa kwa maandishi na yatawekwa saini na wajumbe wote waliyokuwepo Zanzibar wakati huo lakini wasipungue wajumbe watano na maamuzi hayo yatakuwa kama maamuzi yaliyoamuliwa katika mkutano, isipokuwa kwamba mjumbe anaweza kutaka, bila ya kujali saini za wajumbe, jambo hilo kuletwa tena katika mkutano unaofuata.

*Kumualika Mtu.*

**4.** Baraza linaweza kumualika mtu yeyote ambaye si mjumbe kuhudhuria majadiliano ya mkutano wa Baraza kama mtaalamu, isipokuwa mtu huyo aliyealikwa hatokuwa na haki ya kupiga kura.

*Kumbu-kumbu za mikutano.*

**5.** Kumbukumbu za mwenendo wa kila mkutano wa Baraza zitathibitishwa na Baraza katika mkutano unaofuata na zitatiwa saini na Mwenyekiti wa Mkutano na Katibu wa Baraza.

Taratibu za Mikutano.

**6.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Baraza litakuwa na uwezo wa kutayarisha taratibu zake zenyewe kuhusiana na mikutano na utekelezaji mzuri wa kazi zake ikijumuisha kamati za Baraza.

Kujiuzulu kwa mjumbe.

**7.**-(1) Mwenyekiti au mjumbe yeyote wa Baraza anaweza, wakati wowote, kujiuzulu kwa kutoa taarifa ya maandishi kwa Mamlaka ya uteuzi na kuanzia tarehe iliyoainishwa kwenye taarifa hiyo au, iwapo hakuna tarehe iliyoainishwa, kuanzia tarehe iliyopokelewa taarifa na mamlaka ya uteuzi, atasita kuwa mjumbe.

(2) Endapo mtu atasita kuwa Mwenyekiti au mjumbe wa Baraza, kama hali itakavyokuwa, kwa sababu nyengine yoyote kabla ya kumaliza muda wake, mamlaka ya uteuzi itamteua mtu mwengine kushika nafasi yake na mtu aliyeteuliwa atashika nafasi kwa kipindi kilichobaki cha mjumbe aliyemtangulia.

(3) Endapo mjumbe yeyote hatohudhuria mikutano mitatu mfululizo ya Baraza bila ya sababu ya msingi, Mwenyekiti wa Baraza atatoa taarifa kwa Waziri kuhusiana na jambo hilo, na Waziri atafuta uteuzi wa mjumbe huyo na atamteua mjumbe mwengine kushika nafasi yake, na mtu aliyeteuliwa atashika nafasi kwa kipindi kilichobakia cha mjumbe aliyemtangulia.

Nafasi kuwa wazi

**8.**-(1) Nafasi ya mjumbe wa Baraza itakuwa wazi :

(a) kwa kufariki;

(b) ikiwa mjumbe, bila sababu ya msingi, ameshindwa kuhudhuria mikutano mitatu mfululizo ya Baraza;

(c) ikiwa mjumbe amejiuzulu au amekosa sifa ya ujumbe wa Baraza; au

(d) ikiwa mjumbe amekosa uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya kiafya ya kimwili au kiakili.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii kuhusiana na akidi, Baraza linaweza kuendelea bila ya kujali kuwa wazi kwa nafasi ya mjumbe miongoni mwa wajumbe na hakutakuwa na jambo au taratibu za Baraza zitakazokuwa batili kwa sababu ya kukosekana kwa uteuzi wa mtu anayekusudiwa kuwa mjumbe.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 6 Aprili, 2020.

..........................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***